USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI


# MIFUMO YETU

Jarida la Mifumo ya TEHAMA ya TAMISEMI

TOLEO NA. 4 • FEBRUARI-APRILI, 2018




# Mapinduzi ya Upatikanaji wa Taarifa kupitia Mtandao Kiambo (LAN)




*Meneja wa Mifumo ya TEHAMA kutoka Mradi wa PS3, Revocatus Mtesigwa, akionesha 'cabinet' yenye nyaya na vifaa mbalimbali vya mtandao kiambo. (Picha: Jacqueline Sombe wa PS3).*

*Jarida hili limeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).*

*" Jarida hili limefanikishwa kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), chini ya Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3). Ofisi ya Rais -TAMISEMI ndiyo itakayowajibika na matokeo ya kazi hii. Jarida hili ni maoni ya Ofisi ya Rais—TAMISEMI, na si lazima liwakilishe maoni ya USAID au Serikali ya Marekani"*

USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

**USAID/TANZANIA UIMARISHAJI WA MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA**

UHURU NA UMOJA

# Bodi ya Uhariri


## Mwenyekiti

*Eng. Mussa Iyombe*
*Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais, TAMISEMI*

## Wajumbe

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Baltazar Kibola – TAMISEMI*
*Rebecca Kwandu – TAMISEMI*
*Desderi Wengaa – PS3*

## Waandishi

*Atley Kuni – TAMISEMI*
*Angela Msimbira – TAMISEMI*
*Gladys Mkuchu – PS3*
*Jacqueline Sombe – PS3*

## Mhariri Mkuu

*Leah Mwainyekule – PS3*

## Wahariri

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Rebecca Kwandu – TAMISEMI*
*Angela Msimbira – TAMISEMI*

## Msanifu Kurasa

*Leah Mwainyekule – PS3*



## Jarida hili hutolewa na:

*Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-TAMISEMI*
*S.L.P 1923*
*Dodoma-Tanzania*
*Simu: (+255) 26 -2321234*
*Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz*
*Tovuti: www.tamisemi.go.tz*
*Blog: blog.tamisemi.go.tz*

## Ndani ya Jarida Hili:

**Tahariri…………………………………………………………………………….uk 6**

**Maana ya Mtandao Kiambo na Faida Zake………………………………….uk 7**

**Miundombinu ya Mtandao Kiambo Yabadilisha Utendaji..………………...uk 8**

**Tarime Yaanza Kutumia Mifumo kwa Urahisi..……………………………..uk 10**

**Mfumo wa Watumisi Si 'Umiza Kichwa' Tena.……………...………………uk 11**

**Miundombinu Chakavu Yabadilishwa Magu……………...…………………uk 12**

**PS3 Yaimarisha Ufanisi wa Mifumo……………………….….…………....uk 13**

**Ucheleweshwaji Taarifa Wafika Kikomo Kondoa..……………...……….……uk 14**

**LAN Yaunganisha Idara Kuhudumia Wananchi Buchosa…....…………….uk 15**

**LAN Yapunguza Athari Katika Mapato Kwimba…………….……………..uk 16**

**Mtandao Kiambo Mkombozi kwa Halmashauri Mpya……………………...uk 17**

*TAHARIRI:*

# Ni Mapinduzi ya Kielektroiki katika Utendaji Kazi Wetu

Kwa muda mrefu tumekuwa tukishuhudia ucheleweshaji na kusuasua kwa majukumu ya kila siku katika Halmashauri nyingi nchini. Hili halikutokana na uzembe wa watendaji, bali lilitokana na ukweli kwamba matumizi ya kielektroniki hayakuwa rafiki.

Hayakuwa rafiki kwasababu kuu mbili: zipo Halmashauri ambazo zilikuwa na vifaa duni vya kuweza kufanikisha kupatikana kwa mtandao wa kielektroniki; na pia zipo Halmashauri ambazo hazikuwa zimeunganishwa kabisa na mtandao wa kielektroniki.

Nyingi ya Halmashauri ambazo hazikuwa kabisa na mtandao wa kielektroniki ni zile mpya ambazo zilikuwa zimemegwa kutoka Halmashauri zingine. Upya wao ulimaanisha kwamba vitu vingi vilitakiwa kuwa vipya, ikiwemo mawasiliano ya kimtandao. Hata hivyo, sote tunafahamu kwamba suala hilo lisingeweza kufanyika kwa haraka, kwani linahusu utaalam pamoja na kutengwa kwa fedha za kulisababisha lifanikiwe.

Kwa sasa hali imebadilika, na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), kwa kushirikiana na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), tumefanikiwa kulipunguza tatizo hilo kwa asilimia kubwa. Kwa kushirikiana na wadau wetu tumeweza kufunga/kuimarisha mtandao kiambo *(Local Area Network – LAN)* katika Halmashauri ziizokuwa na uhitaji, na sasa utendaji kazi katika Halmashauri hizi umerahisishwa.

Urahisi huu unatokana na ukweli kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa hutegemea sana kufanya kazi kupitia mifumo mbalimbali iliyoundwa. Ipo mifumo kama vile Mfumo wa Takwimu za Elimu Nchini (BEMIS), Mfumo wa Rasilimali Watu (LAWSON), Mfumo wa Fedha (FFARS & EPICOR), Mfumo wa Taarifa za Hospitali (GoT-HoMIS), Mfumo wa Kukusanya Mapato (LGRCIS), Mfumo wa Mipango na Bajeti (PlanRep) pamoja na Mfumo wa Tovuti za Serikali (GWF). Mifumo yote hii hutegemea uwepo wa mtandao wa kielektroniki, na hivyo hutegemea uwepo wa mtandao kiambo.

Zamani watendaji wa Serikali walilazimika kutumia simu zao za mkononi ili kuweza kuingia kufanya kazi katika mifumo mbalimbali, na maeneo mengine ambako simu za mkononi zilipatikana kwa shida, basi watendaji waliteseka zaidi na kujikuta hata wakisafiri kwenda wilaya nyingine na mkoa mwingine, ili waweze kufanya kazi walizotakiwa kuzikamilisha.

Ndani ya jarida hili la *Mifumo Yetu*, utapata simulizi mbalimbali zinazohusiana na namna watendaji wa Halmashauri walivyokuwa wakipata changamoto za utendaji kutokana na ukosefu wa mtandao kiambo, na namna sasa wanavyotarajia kufanya kazi kwa wepesi zaidi baada ya mtandao huo kufungwa kwenye maeneo yao. Ni simulizi zinazodhihirisha muitikio wa kufanya kazi kwa kasi ya Serikali ya awamu ya tano, na namna OR-TAMISEMI pamoja na wadau wa maendeleo tunavyoshirikiana katika kutimiza ndoto ya kuimarisha mifumo ya sekta za umma.

Naomba niwakaribishe kusoma jarida hili, na niwatakie ufanyaji kazi mwema wa kasi zaidi na ari zaidi.

**Eng. Mussa Iyombe**
**Katibu Mkuu, OR-TAMISEMI**

## KUTOKA DODOMA:

# Maana ya Mtandao Kiambo na Faida Zake

Mtandao Kiambo (LAN) ni miundombinu ya kimkakati inayounganisha vifaa vya TEHAMA (kompyuta, printer. Scanner, nk.) za taasisi moja ndani ya jengo moja au zaidi. Vifaa vya TEHAMA vilivyopo katika LAN moja vinaweza kuwasiliana, na hivyo taarifa na data kuweza kuwasilishwa.


Ofisi moja inaweza kuwa na LAN zaidi ya moja (jengo moja-LAN moja) na baadae kuunganishwa na LAN moja kubwa (Extended LAN)

Faida za uwepo wa Mtandao Kiambo uliosanifiwa na kujengwa vyema ni pamoja na:

- Kurahisisha mawasiliano kutoka Idara/Kitengo kimoja na kingine; Idara/Kitengo na wadau wa taasisi kupitia ama *'internet'* au *'extranet'*.
- Kuwezesha matumizi shirikishi ya rasilimali za TEHAMA (Shared ICT resources) kama *'printer,' 'photocopier,'* mifumo n.k
- Kupunguza gharama zitumikazo katika mawasiliano ambapo hupunguza ulazima wa kutoa nakala ngumu
- Kupunguza muda wa kutoka Idara/Kitengo/Dawati moja kwenda lingine
- Kuongeza matumizi madhubuti ya *'intercom'*
- Kuongeza ufanisi wa watumishi kwa kupata kiurahisi nyaraka/taarifa zilizopo katika *'file server'* au *'data repository'* ya taasisi
- Kuongeza usalama, kwani LAN hulindwa na chochote kitokacho nje ya taasisi kwa njia ya mtandao, huchunguzwa na kuzuia au kupitishwa

Faida zitokanazo na LAN zilishindwa kupatikana kutokana na ama LAN kutokuwepo kabisa au kutokutosheleza au kutokuwepo kulingana na viwango vinavyotakiwa. Ofisi ya Rais-TAMISEMI pamoja na PS3 imefanyia kazi suala hili kwa kutumia watumishi wake. Matumizi ya watumishi wa Serikali katika kusanifu, kujenga na kuimarisha LAN yameongeza ujuzi, umiliki, ari na hamasa ya kufanya kazi zaidi.

**"LAN ndiyo msingi wa matumizi ya mifumo ya TEHAMA. Pasipo LAN, hakuna mfumo."**



*Afisa TEHAMA wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa, Edward Mwasakafyuka, akiipata vema mifumo ya Serikali baada ya mtandao kiambo kufungwa kwenye Halmashauri yake (Picha: Jacqueline Sombe, PS3).*

## *KUTOKA DODOMA:*

# Miundombinu ya Mtandao Kiambo Yabadilisha Utendaji katika Mikoa na Halmashauri



***Afisa TEHAMA kutoka OR-TAMISEMI, Antidius Anatory (kulia), akimuonesha Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu—Sera na Uratibu, Prof. Faustine Kamuzora 'cabinet' ya kuhifadhi vifaa mbalimbali vya mtandao kiambo katika ofisi za TAMISEMI mjini Dodoma (Picha: Atley Kuni wa OR-TAMISEMI).***

Miundombinu ya Mtandao kiambo *'Local Area Network'* (LAN) imebeba chachu ya mabadiliko chanya tangu kuanza kwa Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), ambapo jumla ya Halmashauri 73 kati ya 93 za Mradi – sawa na asilimia 74.2 zimefungiwa na kuboreshewa miundombinu.

Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ni miongoni mwa wanufaika wakubwa wa uwekaji wa miundombinu ya Mtandao Kiambo, na kuwarahisishia kufanya kazi watendaji wa Mamlaka hizo.

Akihojiwa na Jarida hili, Mkurugenzi Msaidizi wa Miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kutoka Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Baltazar Kibola, amesema mbali ya jitihada ambazo serikali ilikuwa inachukua katika uboreshaji wa miundombinu kwa kutumia fedha zake za ndani, kazi ilikuwa ngumu kutokana na ufinyu wa bajeti na vipaumbele vya Serikali.

Amesema kwamba katika mwaka wa fedha wa 2011/12, ufungaji wa miundombinu ya mtandao kiambo ulihusisha Halmashauri 47 pekee, huku ikijielekeza katika vyumba vya mfumo wa kielektroniki wa malipo katika Halmashauri ujulikanao kama Epicor.

"Utakuwa mchoyo wa fadhila usipowataja wenzetu wa PS3 ambao kimsingi wamekuwa chachu ya mabadiliko. Kila mfumo ambao ulikuwepo na mingine iliyoanzishwa ilihitaji miundombinu ya LAN katika eneo husika, jambo ambalo tungelimaliza lakini kwa kuchukua muda," amesema Kibola na kuongeza kwamba ujio wa mradi wa PS3 umekuwa msaada wa manufaa kwa kuendelea kutatua tatizo na kufikia takribani asilimia 74.2%

***Inaendelea ukurasa wa 9***

# Miundombinu ya Mtandao Kiambo Yabadilisha Utendaji

*Inatoka ukurasa wa 8*

Ameongeza kwamba hivi sasa OR-TAMISEMI inasimamia mifumo saba ambayo ni Mfumo wa Malipo (EPICOR na TISS), Mfumo wa Takwimu za Elimu Nchini (BEMIS), Mfumo wa Rasilimali Watu (LAWSON), Mfumo wa Fedha (FFARS), Mfumo wa Taarifa za Hospitali (GoT-HoMIS), Mfumo wa Kukusanya Mapato (LGRCIS), Mfumo wa Mipango na Bajeti (PlanRep) pamoja na Mfumo wa Tovuti za Serikali (GWF). Mifumo yote hii inategemea miundombinu imara ya mtandao kiambo.

Mkurugenzi Kibola ameeleza kwamba uwepo wa Mradi wa PS3 umesaidia kuleta mabadiliko makubwa katika suala zima la uimarishaji miundombinu ya mtandao Kiambo katika Halmashauri zote 93 zilizo chini ya ufadhili wa Mradi huo, kwani zimewezeshwa sehemu ya vifaa na tayari zina miundombinu kiambo.

Ameongeza kwamba licha ya PS3 kufanya kazi katika Mikoa 13 na Halmashauri 93 nchini, bado mradi huo umezingatia mahitaji ya jumla ili kuweza kwenda kwa pamoja na Halmashauri ambazo ziko nje ya mradi.

Amefafanua zaidi kwamba uwepo wa miundombinu ya mtandao Kiambo kumesaidia urahisishaji wa shughuli, kutoingiliana kwa ratiba za utendaji kazi, lakini pia kutoa matokeo chanya yenye tija kwa taifa.

"Narudia tena kusema kila idara hivi sasa ina miundombinu ya LAN katika eneo lake. Kwa mantiki hiyo, mtu awe wa idara ya Mipango au Utawala, halazimiki tena kutembea kufuata huduma idara nyigine. Sambamba na hilo, viongozi katika ofisi zao wanaweza kufuatilia kila idara wakiwa katika dawati," anaeleza Kibola.

Akizungungumzia urahisi wa utendaji kazi, Mkurugenzi huyo amesema kumekuwa na utendajikazi kazi wa haraka unaotokana na miundombinu hiyo kutandaa maeneo tofauti-tofauti ya ofisi, na suala la kuchelewesha taarifa limepungua sana ikilinganishwa na awali.

"Kulikuwa na visingizio vingi kabla ya uimarishaji wa miundombinu, lakini sasa vimepungua. Zamani ilikuwa ukiomba taarifa unaweza kujibiwa kwamba hakuna mtandao, ila sasa hali hiyo imepungua sana ukilinganisha na hapo awali," anafafanua.

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera na Uratibu, Profesa Faustine Kamuzora, anasema kuna umuhimu wa kuunganishwa kwa mifumo ya TEHAMA na Takwimu katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma. Ameelezea pia umuhimu wa ushirikiano kati ya wataalam wa OR-TAMISEMI katika ujenzi na maboresho mbalimbali ya TEHAMA na takwimu ili kuwaletea wananchi maendeleo.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Uratibu shughuli za Serikali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Obey Assey, amepongeza jitihada mbalimbali za wadau wa maendeleo wanaoshirikiana na Serikali, ikiwemo PS3, hususan suala zima la uimarishaji wa mifumo.

Tangu mwaka 2015, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) kupitia mradi wa PS3 limefanikiwa kuimarisha baadhi ya mifumo katika Mikoa 13 na Halmashauri 93 nchini. Mradi huo wa miaka mitano utaendelea na shughuli za uimarishaji wa mifumo na hadi utakapomaliza muda wake mwaka 2020.

***Atley Kuni na Angela Msimbira, OR-TAMISEMI***



*Mkurugenzi Msaidizi wa Miundombinu ya TEHAMA kutoka OR-TAMISEMI, Baltazar Kibola (Picha ya maktaba).*

*KUTOKA MARA:*

# Tarime Yaanza Kutumia Mifumo kwa Urahisi

Halmashauri ya Mji wa Tarime imefanikiwa kuanza kutumia kwa urahisi mifumo mbalimbali katika utekelezaji wa kazi zao, kutokana na kufungwa kwa mtandao kiambo (LAN) katika Halmashauri hiyo.

Hayo yamesemwa na Afisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa Halmashauri hiyo, Ngobai Mwisarya, wakati wa mahojiano maalum kuhusu faida za kuanza kutumika kwa LAN ambayo awali ilipatikana katika Idara ya Fedha pekee.



*Afisa TEHAMA wa Halmashauri ya Mji wa Tarime, Ngobai Mwisarya, akizungumza wakati wa moja ya warsha za mafunzo ya mfumo wa tovuti mjini Musoma (Picha: Jacqueline Sombe wa PS3)*

"Shukrani kubwa ziwaendee Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma na TAMISEMI kwa kuona changamoto iliyokuwa inatukabili na kuchukua hatua za haraka na sasa tumepata mtandao kiambo ambao umerahisisha mawasiliano na uendeshaji wa shughuli za Halmashauri katika idara zote," amesisitiza Mwisarya.

Kwa mifumo mbalimbali inayotumika katika Halmashauri, Mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS) katika Halmashauri hiyo unatakiwa kutumiwa na Idara ya Fedha, Biashara, Idara ya Ujenzi, Idara ya Mipango na Mkurugenzi wa Halmashauri.

Kutokana na kukosekana kwa LAN katika idara nyingine iliwalazimu watumishi wengine kuhamia katika ofisi ya Idara ya Fedha ili waweze kutekeleza majukumu yao, hali iliyozorotesha utendaji wao na huduma walizotakiwa kutoa kwa wananchi.

Naye Afisa Utumishi wa Halmashauri ya Mji wa Tarime, Elias Ngwalu, ameelezea kufurahishwa kwake na kuwepo kwa mtandao kiambo katika ofisi za idara yake kwani itawasaidia kufanya kazi kwa ufasaha na kuepuka kulimbikiza kazi zinazohusiana na mfumo. Vilevile, amesema kwamba miundombinu hiyo itasaidia kuwahudumia watumishi katika masuala yote yanayohusu mfumo wa LAWSON.

Mbali na taarifa za kimfumo, Idara ya Rasilimali Watu ilihitaji sana kuwepo kwa mtandao wa kawaida ili kuweza kutuma na kupokea barua pepe kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora (Utumishi) zinazohusiana na masuala ya watumishi katika Halmashauri ya Mji wa Tarime.

Kwa upande wake, Mhasibu wa Halmashauri ya Mji wa Tarime, Masanja Sabuni, ameushukuru Mradi wa PS3 kwani ingawa walikuwa na mtandao kwa ajili ya kufanya kazi za EPICOR, bado haukuwa katika ubora na hivyo kuchelewesha baadhi ya kazi.

"Kwa kazi hii ambayo imefanyika kwa siku chache na yenye matunda, nipende kusema kwamba PS3 imetupunguzia mzigo mkubwa ambao ingetugharimu muda mrefu na gharama kwa Halmashauri," anasema Sabuni.

Halmashauri ya Mji wa Tarime ni moja kati ya Halmashauri mpya. Ilianzishwa Julai, 2013 huku ikikabiliwa na changamoto kubwa ya miundombinu ya mifumo ambayo ilikuwa haijitoshelezi kwa watumishi kutumia kwa kazi mbalimbali zilizohitaji mtandao kama vile LAWSON, EPICOR, na BEMIS.

***Jacqueline Sombe, PS3***

*KUTOKA NJOMBE:*

# Mfumo wa Watumishi Si 'Umiza Kichwa' Tena



*Eneo la Wilaya ya Makete linavyoonekana (Picha: tanzaniatoday.co.tz)*

Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi kirefu zimekuwa na changamoto ya ufanyaji kazi na matumizi ya mifumo ya Serikali. Hii imechangiwa na kutokuwepo kwa mtandao wenye kuwezesha kupatikana na kutumia mifumo kwa urahisi na hivyo kufanya utendaji kazi kupitia mifumo hii kuwa na vikwazo.

"Tumekuwa na changamoto za utendaji kazi katika mfumo wa watumishi katika Halmashauri (LAWSON) kutokana na kutokuwepo kwa mtandao unaowezesha upatikanaji wa matumizi ya mfumo huu. Hii ilitulazimu kufanya kazi usiku wa manane pale ambapo mtandao unakuwa hauna watumiaji wengi ili tu kuwezesha kukamilisha kazi ambapo pia nayo haikuwa ya uhakika sana kwasababu iliwezesha ukamilishaji kazi kwa kiasi tu na kwa kutumia muda mrefu," anasema Benedict Sailes, Afisa Utumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Makete.

Sailes anaongeza kwamba wakati wa kuajiri watumishi wapya na kuweka taarifa zao katika mfumo wa LAWSON, kulikuwa na changamoto kubwa katika ukamilishaji wa zoezi hilo ili waajiriwa waweze kuripoti katika vituo vyao vya kazi. Kutokana na changamoto ya mitandao iliyokuwepo mwaka 2015 iliwalazimu kusafiri kwenda mkoa mwingine ili tu kuweza kukamilisha kazi kwakuwa kulikuwa na upatikanaji wa mtandao kwa urahisi na hivyo kuweza kufanya kazi kwa wepesi kidogo.

"Kuna wakati tulishawahi kusafiri kutoka huku Makete ambayo iko mkoa wa Njombe, hadi mkoa wa Mbeya kwa ajili ya kuweza kupata mtandao ambao angalau ulikuwa na uhakika kidogo kuliko ule tulioKuwa nao sisi. Tulilazimika kukaa mbali na familia, na hata kazi za ofisini kwetu zilisimama ili tuweze kukamilisha zoezi lile," anakumbuka.

Sailes anaishukuru Serikali pamoja na Mradi wa PS3 kwa kuja na suluhisho katika kutatua changamoto hiyo na kuwezesha ufungwaji wa mtandao kiambo, yaani LAN, ambao unawezesha upatikanaji wa mtandao kwa urahisi na hivyo kuwezesha upatikanaji wa mifumo ya Serikali kwa haraka na kukamilisha utendaji kazi.

Kabla ya kuwepo kwa LAN, taarifa za watumishi wakati wa kuajiriwa, kupandishwa vyeo na mishahara ilikuwa inatumia muda mrefu sana kuingizwa katika mfumo wa LAWSON na hii ilisababisha watumishi kuchelewa kufika katika vituo walivyopangiwa, jambo lililosababisha huduma kuahirishwa katika vituo vya kutolea huduma kama vile vituo vya afya kwa watumishi wa afya na vilevile kwa walimu katika shule za msingi na sekondari.

Sailes anaeleza zaidi kwamba uwepo wa LAN katika Halmashauri umeboresha utendaji kazi na sasa wanaweza kuingiza taarifa za watumishi kwa muda mfupi na hivyo kushughulikia kwa haraka masuala ya watumishi. Jambo hili, anaeleza, linasaidia kuleta motisha kwa watumishi lakini vilevile kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi kutokana na kuwepo kwa watoa huduma vituoni mwao.

***Gladys Mkuchu, PS3***

### KUTOKA MWANZA:

# Miundombinu Chakavu Yabadilishwa Magu

Licha ya kuwepo kwa mtandao kiambo (LAN), Halmashauri ya Wilaya ya Magu ilikuwa inakumbwa na changamoto ya mtandao kusuasua, hivyo kusababisha kazi mbalimbali za mifumo zilizohitaji mtandao kukwama. Kazi hizo zilihusisha shughuli kama vile za tovuti, za kifedha na rasilimali watu.

Mtaalamu wa mifumo katika Halmashauri hiyo, Surumbu Emmanuel, anakiri kuwepo kwa miundombinu ambayo ilikuwa chakavu, huku akifafanua kwamba awali mtandao huo ulikuwepo kwenye ofisi kumi tu, wakati mahitaji ni ofisi 15.

Surumbu anakiri kwamba zaidi ya shilingi milioni 15 ambazo zilitakiwa zibebwe kwenye bajeti ya Serikali katika kuimarisha mifumo ya Halmashauri, hususan suala zima la LAN, sasa zimebebwa na PS3. Mantiki ni kuwa fedha hizo sasa zitaelekezwa kwenye shughuli nyingine za maendeleo ndani ya Halmashauri hiyo.

"Kwakweli hatuna lugha nzuri ya kusema, lakini yatosha kuwashukuru sana PS3. Kabla ya mifumo kulikuwa na ucheleweshaji mkubwa sana wa kazi, mfano watu wa malipo na watu wa mapato walilazimika kutumia sehemu moja kwasababu tu ya uhaba wa miundombinu," anaeleza.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Lutengano Mwalwiba, anaeleza kwamba mifumo ya mawasiliano kama vile tovuti imeweza kuboreshwa na imefanikiwa kuleta manufaa katika sekta ya afya wilayani humo.

"Tulipokea mashuka 150 kutoka kwa mtu aliyetusoma katika tovuti ya Halmashauri, ambayo imesaidia kuokoa fedha kiasi cha shilingi milioni 1.5 ambazo sasa zitaelekezwa kwenye matumizi mengine, hususan katika masuala ya vifaa tiba," anasema.

Mkurugenzi huyo wa Halmashauri anakiri kwamba mashuka 150 yatasaidia katika kutoa huduma kwa wananchi wa wilaya ya Magu.

Naye Sililo Posiano Butoke, Afisa Utumishi katika Wilaya ya Magu, anaeleza kwamba kuwekwa kwa LAN sasa kutaimarisha mifumo, hususan EPICOR na LAWSON, ambayo hapo kabla ilikuwa ikisuasua.

Akiongea kwa shauku, Butoke anaongeza kwamba awali zoezi la kupakua hati ya mshahara lilikuwa likitumia dakika 45 kwa hati moja tu wakati zoezi hilo hutakiwi kuendelea na kazi nyingine yeyote. "Kulikuwa na ugumu mkubwa hapo mwanzo," anasema.

***Atley Kuni, OR-TAMISEMI***



***Mmoja wa mafundi kutoka kampuni ya SoftNet akifunga mtandao kiambo wakati zoezi hilo lia ufungwaji mtandao lilipokuwa linaendlea kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Magu (Picha: Jacqueline Sombe wa PS3).***

## *KUTOKA DAR:*

# PS3 Yaimarisha Ufanisi wa Mifumo ya Kitaifa katika Halmashauri

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kwa kushirikiana na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), wamewezesha ufungaji wa Mtandao Kiambo (LAN) katika Halmashauri nchini. Hii ni kutokana na mahitaji yaliyopo katika Serikali Kuu juu ya uimarishaji wa mifumo ya kitaifa inayotumika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuunganishwa moja kwa moja na OR-TAMISEMI.

"Awali kulikuwa na changamoto mbalimbali kutokana na kuwepo kwa mtandao kiambo ambao umepitwa na wakati na kusababisha kasi ya utendaji kazi wa mifumo kuchukua muda mrefu katika kukamilisha kazi mbalimbali katika Halmashauri na mara nyingine kusababisha ucheleweshwaji wa huduma kwa wananchi," amesema Revocatus Mtesigwa, Meneja wa Mifumo ya TEHAMA kutoka PS3.

Kwasababu hiyo, idara chache ndani ya Halmashauri ndizo zilizokuwa na LAN na hivyo kusababisha ofisi za idara zingine ambazo nazo hutumia mifumo, kupata changamoto katika kukamilisha kazi mbalimbali zinazowalazimu kutumia mtandao. Mara kadhaa pia maafisa wa Halmashauri zingine ambazo hazikuwa kabisa na upatikanaji wa mtandao walilazimika kusafiri kwenda kwenye Halmashauri za karibu kuweza kupata huduma hiyo.

Revocatus ameeleza kwamba changamoto hii imeonekana katika Halmashauri mpya ambazo zimegawanywa kutoka kwenye Halmashauri zingine, na kuwa na changamoto ya kutokuwa na vifaa vya kutendea kazi ikiwemo upatikanaji wa LAN. Mfano mmojawapo ni wa Halmashauri ya Mji wa Kondoa iliyoko mkoa wa Dodoma, ambao iliwabidi maafisa wake wawe wanakwenda kufanyia kazi mifumo mbalimbali kwenye Halmashauri mama ya Wilaya ya Kondoa. Mara nyingine walilazimika kukaa muda mrefu ili kuweza kukamilisha kazi hizo na hivyo kusababisha Halmashauri kushindwa kukamilisha majukumu yao kwa muda unaotarajiwa.

"Kwa kubaini changamoto hizi pamoja na mahitaji yaliyopo katika kuimarisha mifumo mbalimbali serikalini, OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na PS3 imefanikiwa kufunga LAN zenye uwezo wa teknolojia ya kisasa katika Halmashauri zaidi ya 65 nchini. Halmashauri zilizobaki ni zile za Manispaa na Jiji ambazo tayari kupitia mradi wa GOVNET wameweza kufungiwa LAN na tayari zinafanya kazi," ameeleza Revocatus.

Ametoa shukrani kwa ushirikiano ulioonyeshwa na baadhi ya Halmashauri ambazo ziliona umuhimu wa kuimarisha utendaji kazi wa mifumo ili kuharakisha utendaji kazi ambao utachochea huduma za haraka kwa wananchi. Halmashauri hizo zimeweza kutenga fedha na kufunga LAN katika ofisi za idara zote ndani ya Halmashauri zao.

"PS3 imewezesha ufungaji wa LAN katika ofisi za idara zinazohusika na mifumo mbalimbali kama vile Mfumo wa Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma (IFMIS-Epicor), Mfumo Shirikishi wa Usimamizi wa Watumishi (HCMIS-Lawson), Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri (LGRCIS), Mfumo wa Idara ya Elimu (BEMIS), Mfumo wa Uhasibu na Utoaji Taarifa kwa Vituo vya Kutolea Huduma (FFARS) pamoja na mifumo mingine mbalimbali inayotumiwa na Idara tofauti katika Halmashauri," ameeleza Mtesigwa.

Kufungwa kwa mtandao kiambo kwenye ofisi za Halmashauri kutasaidia sana kuokoa mapato ya Halmashauri kwasababu mifumo ya manunuzi na matumizi itaweza kufanya kazi kwa usanifu na kutoa taarifa kamili za makusanyo ya mapato, na Serikali itaweza kufanya ufuatiliaji wa rahisi kupitia mifumo iliyounganishwa katika Serikali Kuu.

***Gladys Mkuchu, PS3***



*Meneja wa Mifumo ya TEHAMA wa PS3, Revocatus Mtesigwa (kulia) akitoa maelekezo kuhusu ufungwaji wa mtandao kiambo katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu (Picha: PS3)*

*KUTOKA DODOMA:*

# Ucheleshwaji Taarifa Wafika Kikomo Kondoa

Kwa zaidi ya miaka mitatu, Idara ya Mipango katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma imekuwa na changamoto ya mtandao wa kielektroniki, suala ambalo liliwalazimu watumishi wa idara hiyo kufikia hatua ya kutumia pesa zao za mfukoni kununua vifurushi vya intaneti katika simu ili kuweza kufanya kazi, ingawa hilo lilikuwa si suluhisho la kudumu.



*Mkuu wa Ofisi ya TEHAMA kutoka Halmashauri ya Jiji la Tanga, Athuman Pemba (kulia) akisaidiana na mmoja wa mafundi kutoka SoftNet kufunga mtandao kiambo katika moja ya Halmashauri nchini (Picha: Jacqueline Sombe, PS3).*

Mchumi kutoka Halmashauri hiyo, Andrew Nguni, anaeleza kwa undani ugumu ambao walikuwa wanaupata kabla ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kushirikiana na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) kufunga mtandao kiambo (LAN) katika ofisi hiyo. Mpaka sasa, mtandao huo umekuwa na manufaa makubwa kwa idara na Halmashauri kwa ujumla.

"Idara yetu hutakiwa kutuma mkoani ripoti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika kila robo ya mwaka, ambayo tarehe ya mwisho huwa tarehe 15 ya mwezi unaofuata baada ya robo ya mwaka, na ripoti hizo hutumwa kwa njia mtandao. Hata hivyo, kutokana na tatizo la mtandao tuliwahi kupewa adhabu *'penalty'* baada ya tathmini ya mwaka kufanyika na kuonekana kuwa tulichelewa kutuma ripoti hiyo kwa kuzingatia tarehe ya mwisho kutumwa," anaeleza Ndugu Nguni.

Pia, kukosa mtandao kuliifanya Idara ya Mipango kuchelewa kupata taarifa za maelekezo ya kikazi kutoka mamlaka ya juu (mkoani), kwani si kila mtu kutoka huko hupiga simu ama kutuma ujumbe kwa baruapepe au simu kueleza kwamba kuna taarifa zimetumwa. Kutokana na hilo, ilibidi idara isubiri maelekezo hayo kufika kwa njia ya posta, hivyo hufika kwa kuchelewa.

Akiwa mwenye furaha, Nguni anasema kwamba tangu kufungiwa mtandao katika ofisi hiyo, idara imeweza kutuma ripoti ya miradi ya maendeleo hata kabla ya tarehe ya mwisho kufika na baada ya tathmini kufanyika waliweza kupata alama kwa asilimia 88 licha ya kwamba wapo katika mazingira ya vijijini ambayo yanaweza yasiwe rafiki kwa mtandao. Hata hivyo, kwa msaada wa kufungiwa mtandao kiambo, wamefanikiwa.

Kwa kufungiwa mtandao wa LAN katika Idara ya Mipango, Ngumi anaeleza kwamba kwa sasa Idara hiyo inafanya majukumu yake kikamilifu kwa kupata maagizo kutoka juu kwa wakati, pamoja na kuunganishwa na kutumia vema mfumo wa uandaaji wa bajeti na mipango (PLANREP), ambao pia unafanya kazi kwa kutegemea mtandao.

Naye afisa TEHAMA wa Halmashuri hiyo, Christopher Kyando, anaeleza kwamba mbali na ofisi ya Mipango ambayo ndio ilikuwa na uhitaji mkubwa wa mtandao katika Halmashauri hiyo, ofisi za Vitengo vya Sheria na Uchaguzi nazo zimefanikiwa kupata mtandao wa LAN. Kutokana na hilo, LAN hii iliyofungwa imesaidia hata kupata mtandao kwa matumizi mengine ya ofisi kama kutuma na kupokea baraupepe.

"Idara ya Mipango hapa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kwa muda mrefu imekuwa na ukosefu wa mtandao licha ya baadhi ya ofisi kama ya Mkurugenzi, Idara ya Fedha, na Kitengo cha Ugavi kuwa na mtandao ambao ulifungwa hapo awali ikiwa ni kwa juhudi za Halmashauri," anasema, na kuishukuru OR-TAMISEMI pamoja na PS3 kwa msaada huo. "Hata mimi kama Afisa TEHEMA imenirahisishia kazi kwani gharama za kutumia fedha kwa simu ya mkononi hata mimi ilinikumba," anaeleza Kyando.

Ufungaji wa LAN kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) umekuwa na manufaa, kwani umeweza kuiongezea Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ufanisi katika kazi na kuifanya kupata sifa bora kutoka katika uongozi mkuu wa Mkoa kwa namna mifumo ilivyoimarika.

***Jacqueline Sombe, PS3***

*KUTOKA MWANZA:*

# LAN Yaunganisha Idara Kuhudumia Wananchi Buchosa



***Meneja wa Mradi wa PS3 Mkoa wa Mwanza, Pelestian Masai (kushoto), akikabidhi vifaa vta mtandao kiambo kwa Afisa TEHAMA wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa, Edward Mwasakafyuka, wakati wa kuanza kwa zoezi la ufungaji mtandao huo (Picha: Jacqueline Sombe, PS3).***

Mradi wa Umarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) umetajwa kuwa kichocheo cha ufanisi katika Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa mkoani Mwanza kutokana na kufungwa kwa mtandao kiambo (LAN) ili kuimarisha mawasiliano ya ndani yanayounganisha idara zote katika kuwahudumia wananchi.

Kauli hiyo imetolewa na Afisa TEHAMA wa Halmashauri hiyo, Edward Mwasakafyuka, wakati wa mahojiano maalum kuhusu utekelezaji wa mradi huo unaolenga kuimarisha usalama utakaosaidia kubaki na taarifa salama endapo kutatokea majanga kama moto, kwakuwa taarifa zote za Halmashauri zitakuwa zimeshaunganishwa katika mfumo wa TEHAMA wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

"Matarajio yetu baada ya kufungiwa LAN ni kwamba huduma zinazotolewa kwa wananchi zitaboreka, itaokoa muda wa kazi uliokuwa unapotea na pia itasaidia kupunguza urasimu katika kutoa huduma kwa Jamii," anasisitiza Mwasakafyuka.

Akifafanua juu ya umuhimu wa kufungwa kwa LAN, Mwasakafyuka anasema kwamba kutokana na kufungwa kwa mtandao huo, gharama za uendeshaji wa Halmashauri zitapungua kwa kiasi kikubwa na fedha zitakazookolewa zitatumika kufanya kazi nyingine za maendeleo. Alitoa mfano kwamba kabla ya kufungwa kwa mfumo huo, watumishi wa Halmashauri walilazimika kusafiri kutoka Halmashauri ya wilaya ya Buchosa kwenda mkoani Mwanza ili kutekeleza baadhi ya majukumu, hali iliyosababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji kwa Halmashauri zilizotokana na kulipia fedha za posho kwa watumishi hao pamoja na usafiri.

Kutokana na kuwepo kwa miundombinu hiyo ya LAN, watumishi sasa watabaki katika vituo vyao vya kazi na kuendelea kutekeleza majukumu yao, hali ambayo inasaidia kuongeza ufanisi.

"Uwepo wa LAN umetuwezesha kuongeza uwazi katika Halmashauri hii, kwani taarifa za kifedha sasa zinapatikana kirahisi ambapo hivi sasa Mkurugenzi wetu hatahitaji tena kuuliza kuhusu taarifa za fedha kwa kila idara kwakuwa ana uwezo wa kuzipitia taarifa hizo akiwa ofisini kwake. Hili litamuongezea uwezo wa ufuatiliaji na pia kumrahisishia usimamizi wa kazi akiwa kama kiongozi wa shughuli za Halmashauri," anasisitiza Mwasakafyuka.

Akieleza kuhusu matarajio yao baada ya kufungiwa mfumo wa LAN, Mwasakafyuka anasema kwamba itaongeza juhudi katika kuwahudumia wananchi kwakuwa mazingira ya kazi yatakuwa rafiki kwa watoa huduma na wananchi wanaofika katika Halmashauri hiyo.

***Na Mwandishi Wetu, PS3***

*KUTOKA MWANZA:*

# LAN Yapunguza Athari katika Mapato Kwimba

Changamoto za mtandao katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba imekuwa ni moja ya kikwazo kilichosababisha athari katika usimamizi wa mapato ndani ya Halmashauri hiyo kupitia Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato katika Halmashauri (LGRCIS).

Changamoto hiyo kwa sasa imeanza kuwa ni ndoto kutokana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) kujihusisha na kuisaidia Halmashauri hiyo kati ya nyingi nchini kuwa na mtandao kiambo, yaani *Local Area Network* (LAN).

Akieleza athari ambazo Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba imekuwa inakumbana nazo kutokana na kukosa mtandao thabiti, Bi. Aziza Omary ambaye ni Mhasibu Mlipaji anasema kwamba miamala ambayo inatumwa kutoka mfumo wa kukusanya mapato hushindwa kufika kwa wakati katika mfumo wa matumizi, hivyo kusababisha mfumo wa malipo kukosa ufanisi.

"Pia athari tulizopata zimekuwa ni pamoja na kukwama kwa utoaji wa huduma kwa wananchi na kuwapelekea kupoteza nauli na rasilimali nyingine, kwani mtu anaweza kufika hapa kufanya malipo ya huduma zitolewazo na Halmashauri lakini kutokana na shida ya mtandao inasababisha mtu huyo kupata huduma kwa kuchelewa sana ama kurudi tena siku ya pili kwa ufuatiliaji," anaongeza Aziza.

Vilevile, ukosefu wa mtandao ulisababisha Halmashauri kupungikiwa mapato kutokana na wateja kuamua kutumia njia zisizo halali ama nje ya utaratibu kwa kuamua kutolipia matangazo au mikutano, ambayo kwa utaratibu wa Halmashauri shughuli hizo hulipiwa kupitia mfumo wa mapato ambao bila kuwa na mtandao husua-sua.



*Mhasibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, Aziza Omary, akifanya kazi kwa urahisi kupitia mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri (LGRCIS), baada ya Halmashauri hiyo kufungiwa mtandao kiambo (Picha: PS3).*

Aziza anaeleza pia kwamba kuna wakati malipo ya safari mbalimbali za watumishi wa Halmashauri hiyo yalikuwa yanashindwa kufanyika kwa wakati kutokana na tatizo hilo, hatimaye kupelekea ucheleweshwaji wa majukumu mbalimbali wanapotakiwa kutoka nje ya vituo vya kazi ama kukwamisha kazi za ndani ya Halmashauri nyingine.

Vilevile, Aziza anasema kwamba changamoto hii imemletea yeye na baadhi ya watendaji lawama nyingi kutoka kwa wateja kutokana na huduma nyingi kukwama, zikiwemo za kushindwa kuchapisha risiti za malipo ya mapato pale mtandao unapokosekana.

Naye Mtendaji wa Kata ya Ngudu, Winifrida Bernard ambaye anashughulika na ukusanyaji wa mapato katika kata ya Ngudu amesema ukosefu wa mtandao katika Halmashauri unamsababishia changamoto katika utendaji wake wa kazi, kwakuwa huhitajika kufika katika Halmashauri ili kufanya majumuisho ya makusanyo ili aweze kupatiwa hati ya malipo *'invoice'*.

"Kwa upande wangu ukosefu wa mtandao umekuwa hatarishi sababu najikuta nimebaki na fedha za makusanyo ambazo taarifa zake zilipaswa kuingizwa katika mfumo, lakini kutokana na kukosa mtandao inanibidi kukaa na fedha hizo hadi mtandao upatikane," anaeleza Winifrida.

Aziza anaishukuru OR-TAMISEMI pamoja na Mradi wa PS3 kwa kuangazia changamoto hizi na kuamua kufunga LAN katika Halmashauri zote za mkoa wa Mwanza, ikiwemo Kwimba, na kuamini kwamba muendelezo wa ushirikiano wa PS3 na Halmashauri yake umeweza kumaliza changamoto ya mtandao kwa upana mkubwa.

***Jacqueline Sombe, PS3***

## *KUTOKA MWANZA:*

# 'Mtandao Kiambo Mkombozi kwa Halmashauri Mpya'

Uwekaji wa mtandao kiambo, yaani *'Local Area Network'* (LAN) katika Halmashauri mbalimbali nchini, hususan Halmashauri mpya, umekuwa ni ukombozi kwa watumishi wa umma ambao wamekuwa wakikumbana na changamoto nyingi wakati wa utendaji wa kazi, hali iliyokuwa inasababisha kukwamisha baadhi ya kazi ama kazi hizo kufanywa katika mazingira magumu.



***Afisa Elimu—Takwimu wa Vifaa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa, Abichi Chacha, akisisitiza jambo wakati wa mahojiano kuhusu kufungwa kwa mtandao kiambo katika Halmashauri yake (Picha: Jacqueline Sombe, PS3).***

Afisa Elimu Takwimu na Vifaa katika Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa Mkoani Mwanza, Abichi Chacha na wanakitengo wenzake katika Idara ya Elimu wamekuwa ni waathirika wakubwa wa kukosekana kwa mtandao huo katika Halmashauri yao.

Chacha anatushirikisha uzoefu wake alioupata na kusema kuwa ni changamoto ambayo si rahisi kuitoa katika kumbukumbu zake za kazi kwani imekuwa ni ya aina yake.

Ilikuwa mnamo mwezi wa nne ambapo Idara ya Elimu ilikuwa katika zoezi la uingizaji wa takwimu za elimu katika mfumo wa BEMIS, mfumo ambao unawezesha kupata taarifa za kila shule katika Halmashauri. Watumishi walipata changamoto kwakuwa uingizaji wa takwimu ulikuwa mgumu kutokana na changamoto ya kukosekana kwa mtandao.

"Tulikuwa tunakesha kuanzia saa mbili usiku hadi saa mbili asubuhi kutokana na changamoto ya mtandao, kwani ilibidi tutumie ofisi ya wahasibu ambayo ndio ofisi pekee hapa Halmashauri ya Buchosa ambayo ilikuwa inaweza kupata mtandao," anaeleza Chacha.

"Kazi hii kuihalisia ilipaswa tuifanye ndani ya siku mbili hadi nne ukizingatia kwamba ilikuwa ni kazi yenye hitaji la kukamilika ndani ya muda maalum. Hata hivyo kutokana na changamoto ya upatikanaji wa mtandao, kazi hii tuliifanya ndani ya siku sita zenye mateso."

Chacha anaendelea kueleza: "Mbali na kukesha, hasa muda wa mchana bado, haikuwa rahisi kufanya kazi hii kutokana na kasi ya mtandao. Wakati mwingine ilikuwa unaweza kuingiza kwenye mfumo shule mbili tu mchana kutwa, hivyo unaweza kuona changamoto kubwa tuliyokuwa nayo hapo awali."

Kufanya kazi muda wa usiku imekuwa ni mazingira hatarishi sana, ukizingatia hali ya ofisi ilivyokuwa. Vilevile, shughuli nyingine za idara hiyo zilikuwa zinakwama sana kutokana na kutopata mtandao,

Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na mradi wa PS3 vimekuwa ni mkombozi kwa Ofisi ya Elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa, kwani Halmashauri hiyo imenufaika na kufungiwa mtandao kiambo ili kukidhi mahitaji ya ofisi hiyo yenye shughuli nyingi za masuala ya elimu huko.

Akieleza faida zitokanazo na kuwekewa LAN katika ofisi ya Idara ya Elimu, Chacha anasema: "Kwa upande wa Idara ya Elimu huduma zitaboreshwa pia kwakuwa wananchi wamekuwa wanafuatilia masuala ya uhamisho wa watoto wao lakini watumishi mara nyingi walikuwa wakikosekana kutokana na kwenda kufuata mtandao mahala pengine. Sasa wananchi hawatakosa tena huduma muhimu za kitaaluma."

***Na Jacqueline Sombe, PS3***

## *MATUKIO YA MAKABIDHIANO YA VIFAA NA MTANDAO KIAMBO KWENYE HALMASHAURI MBALIMBALI NCHINI:*

***Picha zote na Jacqueline Sombe, PS3***













## *MATUKIO YA UFUNGAJI MTANDAO KIAMBO KWENYE HALMASHAURI MBALIMBALI NCHINI:*

***Picha zote na Jacqueline Sombe, PS3***













# MIFUMO YETU